FUNZO LA 24

1. Baada ya mke wa Ibrahamu Sara kufa, Ibrahamu alimfanyia nini Isaka ili kumfariji?
-Ibrahamu alimtafutia mwanawe Isaka mke.

2. Je, jina la mke wake Isaka lilikuwa lipi?
-Rebeka.

3. Je, Mungu alijuaje kila kitu kuwahusu mapacha wa Rebeka kabla wazaliwe?
-Mungu anajua kila kitu kuhusu watu wote.
-Hakuna kisicho wazi kwa Mungu.

4. Je, majina ya wavulana mapacha ambao Rebeka alizaa waliitwaje?
-Esau na Yakobo.

5. Je, Esau alimwamini Mungu?
-La.

6. Je, Yakobo alimwamini Mungu?
-Ndiyo.

7. Je, kwa nini Mungu aliamua kumtuma mwokozi kupitia uzao wa Yakobo?
-Kwa sababu Esau hakumwamini Mungu.

8. Je, Yakobo aliona nini katika ndoto aliyopewa na Mungu?
-Yakobo aliona ngazi.



9. Je, sehemu ya chini ya hio ngazi iligusa wapi?
-Sehemu ya chini ya hio ngazi iligusa ardhi.

10. Je, sehemu ya juu ya hio ngazi ilielekea wapi?
-Sehemu ya juu ya hio ngazi iligusa mbingu.

11. Je, ilimaanisha nini ngazi kugusa ardhi na pia kugusa mbingu?
-Ngazi ilikuwa inaleta mbingu na ardhi pamoja.

12. Je, kwa nini Mungu alimpa Yakobo hii ndoto?
-Mungu alikuwa akimfundisha Yakobo kuhusu Mwokozi ambaye angekuja.

13. Je, Mungu alimfundisha Yakobo nini kuhusu Mwokozi?
-Kama vile ngazi ilivyoleta mbingu na ardhi pamoja, hivyo Mwokozi angewaleta watu wa ardhi pamoja na Mungu wa Mbinguni.

14. Je, kwa nini Mungu hawezi sahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi?
-Kwa sababu Mungu hasahau.
-Kwa sababu Mungu habadiliki.
-Kwa sababu Mungu anatimiza ahadi zake wakati wote.

15. Je, baada ya Yakobo kuishi Harani miaka mingi, Mungu alimwambia nini Yakobo?
-Mungu alimwambia Yakobo atoke Harani na arejee nchi ya Kanaani.

-Je, ni nani aliyemlinda Yakobo na kumrejesha salama kutoka nchi ya Harani hadi Kanaani?

-Mungu.

Tusome Mwanzo 37:1

1-Yakobo akakaa katika nchi aliyosafiri baba yake, katika nchi ya Kanaani.

-Je, jina mpya ambalo Mungu alimpa Yakobo ni lipi?
-Israeli.

Tusome Mwanzo 37:3

3-Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko wanawe wote, maana ni mwana wa uzee wake, akamfanyia kanzu ndefu.

-Je, Yakobo alikuwa na wana wangapi?
-Kumi na wawili.

-Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili lakini alimpenda mmoja wao zaidi ya wengine.

-Je, jina la mwana wa Yakobo aliyempenda zaidi ya wote lilikuwa lipi?
-Yusufu.

-Kwa sababu Yakobo alimpenda Yusufu zaidi, alimtengenezea vazi la kifahari.



-Kwa sababu Yakobo alimpenda Yusufu zaidi ya ndugu zake, ndugu zake walimfikiria vipi Yusufu?

-Walimwonea wivu na pia walimchukia.

-Pia ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu kwa sababu alimwarifu baba yao kila walipofanya jambo mbaya.

Tusome Mwanzo 37:2 & 4

2-Hivi ndivyo vizazi vya Yakobo. Yusufu, aliyekuwa mwenye miaka kumi na saba, alikuwa akichunga kondoo pamoja na ndugu zake; naye alikuwa kijana pamoja na wana wa Bilha, na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. Yusufu akamletea baba yao habari zao mbaya.
4-Ndugu zake wakaona ya kuwa baba yao anampenda kuliko ndugu zake wote, wakamchukia, wala hawakuweza kusema naye kwa amani.

-Je, kwa nini watu huwakasirikia wenzao?
-Je, kwa nini watu huwachukia wenzao?

-Kwa sababu kila mtu amezaliwa akiwa ametengana na Mungu.
-Kwa sababu kila mtu amezaliwa na dhambi ndani ya moyo wake.

-Kwa sababu kila mtu amezaliwa kama mtoto wa Shetani.

-Ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu kwa sababu walizaliwa wakiwa wametenganishwa na Mungu.

-Ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu kwa sababu walizaliwa na dhambi mioyoni mwao.

-Ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu kwa sababu walizaliwa kama watoto wa Shetani.

-Kila mtu amezaliwa akiwa ametenganishwa na Mungu na hatuwezi kujibadilisha.

-Kila mtu amezaliwa na dhambi moyoni mwake na hatuwezi kujibadilisha.

-Kila mtu amezaliwa kama mtoto wa Shetani na hatuwezi kujibadilisha.

-Siku moja, Mungu alimpa Yusufu ndoto.

Tusome Mwanzo 37:5-8

5-Yusufu akaota ndoto, akawapa ndugu zake habari, nao wakazidi kumchukia;
6-akawaambia, Tafadhalini, sikieni ndoto hii niliyoiota.
7-Tazama, sisi tulikuwa tukifunga miganda shambani, kumbe! Mganda wangu ukaondoka ukasimama, na tazama, miganda yenu ikazunguka ikainama mbele ya mganda wangu.
8-Ndugu zake wakamwambia, Je! Kweli wewe utatumiliki sisi? Nawe utatutawala sisi? Wakazidi kumchukia kwa ajili ya ndoto yake, na kwa maneno yake.

-Je, ndoto ambayo Mungu alimpa Yusufu ilikuwaje?



-Katika hiyo ndoto, Yusufu na ndugu zake walikuwa wakifumba mafungu ya nafaka shambani.

-Kisha, mafungu ya ngano ya ndugu za Yusufu yaliinamia fungu la nafaka la Yusufu.

-Kwa sababu ya hio ndoto ambaye Mungu alimpa Yusufu, ndugu zake walimchukia zaidi.

-Muda baadaye, Mungu alimpa Yusufu ndoto nyingine.

Tusome Mwanzo 37:9-11

9-Akaota tena ndoto nyingine, akawaambia ndugu zake, akasema, Angalieni, nimeota ndoto nyingine; na tazama, jua na mwezi na nyota kumi na moja zikaniinamia.
10-Akawaambia baba yake na ndugu zake; baba yake akamkemea akamwambia, Ni ndoto gani hii uliyoiota? Je! Mimi na mama yako na ndugu zako tutakuja tukusujudie hata nchi?
11-Ndugu zake wakamhusudu; bali baba yake akalihifadhi neno hili.

-Je, ndoto ya pili ambayo Mungu alimpa Yusufu ilikuwaje?

-Katika hio ndoto, kulikuwa jua, mwezi na nyota.

-Kisha jua, mwezi na nyota kumi na moja zikamsujudia Yusufu.

-Katika hio ndoto, nani aliyekuwa jua?
-Babake Yusufu.

-Katika hio ndoto, nani aliyekuwa mwezi?
-Mamake Yusufu.

-Katika hio ndoto, nani waliokuwa nyota kumi na moja?
-Ndugu zake Yusufu kumi na moja.

-Je, hizo ndoto mbili zilimaanisha nini?

-Siku moja, Mungu atamfanya Yusufu mkuu, na jamii yake wangemsujudia.

-Je, ni nani aliyejua hatima ya Yusufu na kumuonyesha katika ndoto?
-Mungu.

-Kama vile Mungu alivyojua hatima ya Yusufu, Mungu pia anajua hatima zetu.

-Je, ni kiasi gani ya hatima zetu ambayo Mungu anajua?

-Mungu anajua hatima yetu yote.

-Kwa sababu ya hizi ndoto ambazo Mungu alimpa Yusufu, ndugu zake walimchukia Yusufu zaidi.

-Siku moja Yusufu alienda kuwatembelea ndugu zake malishoni.



Tusome Mwanzo 37:17b-20

17-Basi Yusufu akawafuata ndugu zake akawakuta huko Dothani.
18-Wakamwona toka mbali, na kabla hajawakaribia, wakafanya shauri juu yake ili wamwue.
19-Wakasemezana wao kwa wao, Tazama, yule bwana wa ndoto anakuja.
20-Haya, twende, tukamwue na kumtupa katika birika mojawapo, nasi tutasema, Mnyama mkali amemla; kisha tutaona zitakuwaje ndoto zake.

-Ndugu zake Yusufu walimchukia sana hadi walitaka kumuua.

-Lakini ndugu yake mkubwa Reubeni, aliamua kumwokoa Yusufu.

Tusome Mwanzo 37:21-24

21-Reubeni akasikia akamwokoa katika mikono yao, akasema, Tusimwue.
22-Reubeni akawaambia, Msimwage damu; mtupeni katika birika hii iliyopo nyikani, wala msimguse; ili apate kumwokoa katika mikono yao, akamrudishe kwa baba yake.
23-Ikawa Yusufu alipofika kwa ndugu zake, wakamvua Yusufu kanzu yake, kanzu ile ndefu aliyoivaa,
24-wakamtwaa wakamtupa katika birika; na hiyo birika ilikuwa tupu, hamna maji.

-Je, ndugu zake Yusufu walimfanyia nini Yusufu?

-Walimvua vazi lake na kumtupa katika kisima kikavu.

-Baada ya ndugu yake Yusufu Reubeni kuondoka, ndugu zake wengine walimfanyia nini Yusufu?

Tusome Mwanzo 37:25-28

25-Nao wakakaa kitako kula chakula; wakainua macho yao, wakaona, msafara wa Waishmaeli wanakuja wakitoka Gileadi na ngamia zao, wakichukua ubani na zeri na manemane, wakisafiri kuvichukua mpaka Misri.
26-Yuda akawaambia ndugu zake, Kwafaa nini kumwua ndugu yetu, na kuificha damu yake?
27-Haya, na tumwuze kwa hawa Waishmaeli, wala mikono yetu isimdhuru, maana yeye ni ndugu yetu, na damu yetu. Ndugu zake wakakubali.
28-Wakapita wafanya biashara Wamidiani; basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini; nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri.

-Ndugu zake Yusufu walimuuza kama mtumwa kwa wachuuzi wa watumwa.

-Je, hao wachuuzi wa watumwa walimpeleka wapi Yusufu?
-Walimpeleka Misri.

-Je, ndugu zake walifanya nini Reubeni aliporudi?

Tusome Mwanzo 37:29-31



29-Akarudi Reubeni birikani, kumbe! Yusufu hayumo katika birika, akararua nguo zake.
30-Akarudi kwa ndugu zake, akasema, Mtoto hayuko, nami niende wapi?
31-Wakaitwaa kanzu ya Yusufu, wakachinja mwana-mbuzi, na kuichovya kanzu katika damu.

-Ndugu zake Yusufu walichukua lile vazi, wakamchinja mbuzi na kutumbukiza lile vazi katika damu ya mbuzi.

-Kisha ndugu zake Yusufu wakachukua lile vazi lililotumbukizwa kwa damu ya mbuzi na kumpelekea baba ya Yakobo.

Tusome Mwanzo 37:32-35

32-Wakaenda nayo ile kanzu ndefu, wakamletea baba yao, wakasema, Tumeona hii; basi, utambue kama kanzu hii ni ya mwanao, ama siyo.
33-Akaitambua, akasema, Ndiyo kanzu ya mwanangu, mnyama mkali amemla; bila shaka Yusufu ameraruliwa.
34-Yakobo akararua mavazi yake, akajivika gunia viunoni, na kumlilia mwanawe siku nyingi.
35-Wanawe wote, na binti zake wote, wakaondoka wamtulize, lakini akakataa kutulizwa, akasema, La! Nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu. Baba yake akamlilia.

-Ndugu zake Yusufu walimuuza kama mtumwa.

-Kisha ndugu zake Yusufu wakamdanganya baba yao Yakobo.

-Yakobo alidhani kuwa Yusufu alikufa.

-Ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu.

-Chuki ya ndugu za Yusufu iliwafanya wamuuze kama mtumwa.

-Chuki ya ndugu za Yusufu iliwafanya wamdanganye baba yao.

-Chuki huelekeza kwa dhambi zaidi.

-Je, Yusufu alikufa?
-La.

-Je, Yusufu alikuwa wapi?

-Yusufu alikuwa Misri.

Tusome Mwanzo 39:1

1-Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko.

-Je, wachuuzi wa watumwa walimuuza Yusufu kama mtumwa kwa nani?

-Kwa Potifa.



-Je, Mungu alimuacha Yusufu?
-La.

-Mungu kamwe hawezi kumuacha yeyote anayemwamini.

-Mungu alikuwa na Yusufu wakati huu wote.

-Je, ni nini kilichomfanyikia Yusufu baada ya Potifa kumnunua?

Tusome Mwanzo 39:2-6a

2-Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi; naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri.
3-Bwana wake akaona ya kwamba Bwana yu pamoja naye, na ya kuwa Bwana anafanikisha mambo yote mkononi mwake.
4-Yusufu akaona neema machoni pake, akamtumikia. Naye akamweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na yote yaliyomo akayaweka mkononi mwake.
5-Ikawa tokea wakati alipomweka awe msimamizi juu ya nyumba yake, na vyote vilivyomo, Bwana akabariki nyumba ya yule Mmisri kwa ajili ya Yusufu. Mbaraka wa Bwana ikawa juu ya vyote alivyokuwa navyo katika nyumba, na katika shamba.
6-Akayaacha yote aliyokuwa nayo mkononi mwa Yusufu.

-Ingawaje ndugu za Yusufu walimchukia Yusufu, Mungu hakumwacha.

-Ingawaje ndugu za Yusufu walimuuza Yusufu kama mtumwa, Mungu hakumwacha.

-Kwa sababu Yusufu alimwamini Mungu, Mungu alimbariki Yusufu.

-Siku moja, Potifa alipokuwa ameondoka, jambo fulani lilimfanyikia Yusufu.

Tusome Mwanzo 39:6b-15

6-Wala hakujua habari za kitu cho chote chake, ila hicho chakula alichokula tu.
7-Ikawa baada ya mambo hayo, mke wa bwana wake akamtamani Yusufu, akamwambia, Lala nami.
8-Lakini akakataa, akamwambia mke wa bwana wake, Tazama, bwana wangu hajui kitu kilichowekwa kwangu nyumbani, na vyote alivyo navyo amevitia mkononi mwangu.
9-Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu cho chote ila wewe, kwa sababu wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu?
10-Akawa akizidi kusema na Yusufu siku baada ya siku, lakini hakumsikia alale naye, wala aongee naye.
11-Ikawa, siku moja, akaingia nyumbani atende kazi yake, wala hapakuwa na mtu katika watu wa nyumbani humo ndani;
12-huyo mwanamke akamshika nguo zake, akisema, Lala nami. Yusufu akaiacha nguo yake mkononi mwake, akakimbia, akatoka nje.
13-Ikawa alipoona ya kwamba amemwachilia nguo yake



mkononi mwake, naye amekimbia nje,
14-akawaita watu wa nyumbani mwake, akasema nao, akinena, Angalieni, ametuletea mtu Mwebrania atufanyie dhihaka. Ameingia kwangu, ili alale nami, nikalia kwa sauti kuu.
15-Ikawa, aliposikia ya kuwa nimepaza sauti yangu na kulia, aliiacha nguo yake kwangu, akakimbia, akatoka nje.

-Kwa sababu Yusufu alimwamini Mungu, alikataa kulala na mke wa Potifa.

-Kwa sababu Yusufu alikataa kulala naye, mke wa Potifa alimsujudia Yusufu uongo.

-Je, ni nini kilichofanyika Potifa aliporejea nyumbani?

Tusome Mwanzo 39:16-20a

16-Basi akaiweka ile nguo kwake hata bwana wake aje nyumbani.
17-Naye akamwambia kama maneno hayo, akisema, Yule mtumwa Mwebrania uliyemleta kwetu, aliingia kwangu anidhihaki.
18-Ikawa nilipopaza sauti yangu, nikalia, akaacha nguo yake kwangu akakimbia nje.
19-Ikawa bwana wake aliposikia maneno ya mkewe aliyomwambia, akisema, Mtumwa wako amenitendea mambo kama haya, hasira yake ikawaka.
20-Bwana wake akamtwaa Yusufu, akamtia gerezani,

-Potifa aliporejea nyumbani, aliukubali uongo wa mkewe na kumtia Yusufu gerezani.

-Je, Yusufu alipokuwa gerezani, Mungu alimwacha?
-La.

-Mungu hawezi kumwacha yeyote anayemwamini.

-Mungu alikuwa na Yusufu wakati huo wote.

-Hata Yusufu alipokuwa gerezani, Mungu alikuwa na Yusufu.

Tusome Mwanzo 39:20b-23

20-Mahali walipofungwa wafungwa wa mfalme, naye akawamo humo gerezani.
21-Lakini Bwana akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza.
22-Mkuu wa gereza akawatia mkononi mwa Yusufu watu wote waliofungwa, waliomo gerezani; na yote yaliyofanyika humo ndiye aliyeyafanya.
23-Wala mkuu wa gereza hakuangalia neno lililoko mkononi mwa Yusufu; kwa sababu Bwana alikuwa pamoja naye. Bwana akayafanikisha yote aliyoyafanya.

-Hata kama ndugu zake Yusufu walimchukia, Yusufu alimwamini Mungu.

-Hata kama ndugu zake walimuuza kama mtumwa, Yusufu alimwamini Mungu.



-Hata kama mke wa Potifa alimsujudia uongo, Yusufu alimwamini Mungu.

-Hata kama Yusufu alitiwa gerezani, alimwamini Mungu.

-Je, ni nani aliyemlinda Yusufu?

-Mungu.

-Je, kwa nini Mungu alimlinda Yusufu?

-Kwa sababu Yusufu alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.

-Kwa sababu Yusufu alijua kuwa dhambi yake ingeleta kifo cha milele.

-Kwa sababu Yusufu alitambua kuwa ni Mungu pekee ambaye angemwokoa.

-Kwa sababu Yusufu aliamini kuwa Mungu angemtuma Mwokozi amwokoe.

-Je, unadhani Mungu angemsahau Yusufu gerezani?
-La.

-Katika fundisho lifuatalo, tutasoma kuhusu kile ambacho Mungu alimfanyia Yusufu akiwa gerezani.